## ULEMAVU



Ikiwa wewe ni mtu mwenye ulemavu, unaoonekana au usioonekana (wa kiakili, wa kimwili, au wa kihisia) mtoaji wa nyumba anayeweza kupatikana au wa sasa hapaswi kukuuliza juu ya asili au kiasi cha ulemavu wako. Wala mtu yeyote katika muamala wa kupata makazi hapaswi kuuliza kuhusu ulemavu wa wanafamilia yako, wageni, watu unaojuana nao, au marafiki. Ikiwa ulemavu wa mpangaji unahitaji kuondolewa kutoka sera/sheria au marekebisho ya ujenzi, ili kutumia na kufurahia makao, mpangaji anaweza toa **ombi la makao yanayofaa** (sheria/sera) au **ombi la marekebisho yanayofaa**(wa ujenzi) kwa mtoaji nyumba. Yaani, Katika jengo la vyumba vya kukodisha ambapo mahali pa kuegesha inapeanwa kwa watakaofika kwanza, mtu mwenye ulemavu wa kutembea anaweza kuuliza nafasi iliyohifadhiwa ya kuegesha. Kwa ujumla, kuna gharama ndogo au hakuna inayohusika. Hata hivyo kwa marekebisho (kuweka chuma cha kujishikilia, njia ya viti vyenye magurudumu, n.k.) mpangaji kwa kawaida atalipia gharama ya marekebisho na anaweza kuulizwa afanye hivyo kwa njia ya kitaalamu ya mtenda-kazi. Inawezekana pia kwamba mpangaji atahitajika na mtoaji wa nyumba kurudisha nyumba katika hali yake ya asili.

## HALI YA USTAAFU/KIJESHI

Kuwa mwanajeshi anayefanya kazi au kuacha jeshi kwa heshima hakufai kupunguza machaguo yako ya makazi. “Samahani, siwezi kukodisha kwako —unaweza kuitwa kazini na ukose kumaliza kipindi cha kukodisha” ni ubaguzi wa makazi. Ikiwa umeitwa kazini, una haki ya kusitisha upangaji bila adhabu ya kifedha. Ikiwa una ulemavu unaohusiana na huduma ya kijeshi, unaweza pia kuuliza mtoaji wa nyumba akupe makao inayofaa au afanye marekebisho yanayofaa kama ilivyoelezwa hapo juu.

## HALI YA NDOA

Katika jimbo la WA, watoaji wa nyumba hawaruhusiwi kukataa kukodisha au kutengeneza sheria na masharti tofauti kwa wapangaji kwa sababu mtu ni mseja, yuko kwenye ndoa, ni mjane, ametengana au kutalikiwa. “Samahani, tungependa kukodisha kwako, lakini tungependelea wenzi wa ndoa walio wazuri na ambao wanafanya kazi katika nyumba yetu” inaweza kusababisha malalamiko ya ubaguzi wa makazi.

---

Uwezo wa mtu kukodisha mahali unapaswa kuzingatia vigezo vya maombi, kupita kwa uchunguzi wa mpangaji, (ripoti ya mkopo, historia ya uhalifu, uhakiki wa historia ya kukodisha) na kukidhi majukumu ya kifedha ya kitengo hicho. Makazi yanapaswa kuorodheshwa na kutangazwa tu kwa sifa zake (vyumba vya kulala, bafu, karakana, staha, n.k.) sio kwa “aina” ya watu ambao mtoaji wa nyumba anapendelea (watu wazima, wanandoa, raia wa Marekani, wanawake pekee, n.k.)

---

Ikiwa unafikiria kwamba umebaguliwa katika shughuli ya kupata makazi, wasiliana na:

Ushirikiano wa Usawa wa Makazi wa Northwest
35 W. Main Ave, Suite 250
Spokane, WA 99201

Nambari ya simu. 509-325-2665
1-800-200-FAIR (3247)
Faksi: 1-866-376-6308
www.nwfairhouse.org

Tunaweza kukushauri juu ya machaguo yako na kukutetea. Huduma zetu ni za bure.

Kazi ambayo ilitoa msingi wa chapisho hili iliungwa mkono kwa sehemu na ufadhili chini ya ruzuku kutoka Idara ya Makazi na Maendeleo ya Mjini ya Marekani. NWFHA inawajibika kikamilifu kwa taarifa na tafsiri zilizomo katika chapisho hili. 4/16



# Haki za Usawa wa Makazi




**USHIRIKIANO WA USAWA WA MAKAZI WA NORTHWEST**

(509) 325-2665
1 (800) 200-FAIR (3247)
www.nwfairhouse.org

# Usawa wa Makazi: Ni Haki Yako!

SERIKALI

- Mbari
- Rangi
- Asili ya Kitaifa
- Dini
- Jinsia
- Ulemavu
- Hali ya Familia (watoto katika familia)

JIMBO LA WA

- Hali ya Ndoa
- Mwelekeo wa Kimapenzi/ Kitambulisho cha Kijinsia
- Hali ya Ustaafu/Kijeshi

EQUAL HOUSING OPPORTUNITY

Kama mpangaji katika Jimbo la Washington, Sheria ya serikali ya Usawa wa Makazi (FHA), inakupa ulinzi, nafasi sawa, na makazi bila ubaguzi kwa msingi wa: mbari, rangi, asili ya kitaifa, dini, jinsia, ulemavu na hali ya familia. Katika Jimbo la WA, Sheria ya Jimbo la Washington Dhidi ya Ubaguzi (WLAD) inakupa ulinzi zaidi wa makazi kwa: hali ya ndoa, mwelekeo wa kimapenzi/kitambulisho cha kijinsia, na hali ya ustaafu/kijeshi.

FHA na WLAD hujumuisha sehemu zote za muamala wako wa kupata makazi: utafutaji wako wa makazi, maombi na uchunguzi, makubaliano ya kukodisha, kupata bima ya kukodisha, sheria na masharti ya upangaji wako, kukodisha upya, kukomesha upangaji na harakati ya kuondoka.

Ikiwa utapita vigezo vya uchunguzi wa mtoaji nyumba, na unaweza kulipa amana, kodi na ada zinazohusiana zinazotangazwa, unapaswa kuwa huru kuchagua nyumba I nayokufaa wewe na/au familia yako zaidi.




## MBARI, RANGI, ASILI YA KITAIFA



http://www.understandingrace.org/home.html
Mradi wa Chama cha Anthropolojia cha Marekani

Kukatazwa nyumba, kuzuiliwa kwa maeneo fulani ya jengo la vyumba vya kupangisha au kuelekezwa kwa mitaa ya "watu kama wewe" ni ubaguzi wa makazi. Ukipiga simu kwa tangazo la makazi na kila kitu kinaonekana kupatikana kwenye simu, lakini unapojitokeza kwenye miadi ya kuona nyumba na ghafla haipatikani tena, unaweza kuwa na madai ya ubaguzi wa makazi.



## DINI/IMANI

Matangazo ya makazi yanapaswa kuondoa/kutenga maelezo na mapendeleo yote ya kidini au yasiyo ya kidini. Matangazo yanayohusu kanisa fulani kama kivutio kwa makazi yanaweza kusababisha madai ya usawa wa makazi isipokuwa makanisa yote kwa ukaribu yameorodheshwa kama inavyoweza kugunduliwa kuwa mtoaji wa nyumba anapendelea, anakubali au kukataa "aina" fulani ya watu kuomba.

## JINSIA

Chini ya Sheria ya Usawa wa Makazi, mtoaji wa nyumba anayeweza kupatikana au wa sasa haruhusiwi kuwanyanyasa wapangaji kingono au kuwaomba wapangaji hisani za kingono ili kupata makazi, huduma za makazi (maboresho ya vifaa, nafasi ya maegesho, n.k.) au huduma za wapangaji kama vile kufanya ukarabati, utunzaji wa vifaa, au kukodisha upya.

## HALI YA FAMILIA (watoto katika nyumba)

Sheria ya Usawa wa Makazi inafanya iwe haramu kwa watoaji nyumba kubagua dhidi ya wapangaji wa sasa au wanaotarajiwa ambao wana mtoto/watoto, wanatarajia mtoto, au wanalea watoto wa kupangwa kama wanafamilia zao. Pili, sheria zinazowazuia sana watoto zinaweza kuzingatiwa kama za kibaguzi kwa kuwa viwango vya makazi lazima vitumike kwa usawa awe mpangaji ni mtu mzima au mtoto.

Yaani "Hakuna vitu vya kuchezea vya watoto katika barabara ya ukumbi" ni ya kibaguzi. "Hakuna mali ya kibinafsi katika barabara ya ukumbi" ni sawa.



Kwa kuongezea,familia zilizo na watoto haziwezi kuelekezwa na watoaji nyumba kukodisha tu vitengo vya ghorofa ya chini (kwa sababu "watoto hupiga kelele") au kukataliwa katika majengo yenye sifa maalum (kwa sababu "ni hatari sana kwa watoto") yaani barabara zenye shughuli nyingi, roshani, mabafu ya mvuke, au mahali pa kuotea moto.

Mwishowe, makazi ambayo imetambulishwa mahususi kwa "Wazee Tu" (55+,62+) lazima ikidhi miongozo maalum sana ili kustahili kuepuka sheria hii. Mwenye nyumba ya kibinafsi ambaye anatangaza kwa "watu wazima tu" bila kuzingatia miongozo yote anakiuka Sheria ya Usawa wa Makazi.